KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na Paul Dysinger - Mtaalamu wa Bustani na Kilimo – Tennessee, Marekani

Mtafsiri: Mch. Steven Letta – Mchungaji wa Mtaa wa Tegeta, Dar es Salaam (ECT)

Juma la Kumi na Moja, Juni 5 – Juni 11, 2020

TUFANI INAPOKUPATA PASIPO KUTARAJIA!

Nilikuwa tu ndio nimemweka mtoto wetu wa kiume Ethan ili alale kidogo. Ilikuwa siku nzuri yenye jua. Baadhi ya mawingu yalikuwa yamejikusanya katika jioni ile yenye kiubaridi. Kisha ikanyesha. Na ilinyesha kwa nguvu na kwa kasi.

Ethan alikuwa tu ndio amelala nilipomsikia mke wangu Natasha akiita kutoka sebuleni. Nilitoka chumba cha kulala na kwenda kuchungulia dirishani. Na kitu cha kwanza nilichokitambua ilikuwa ni upepo. Ulikuwa unavuma kwa nguvu sana. Na anga lilikuwa linaanza kuwa na giza zaidi kila muda ulipokuwa unaendelea.

Kisha tukasikia matawi ya miti ikianza kukatika. Khaa, khaa, phuuu! Matawi yalikuwa yanachomoka kutoka kwenye mti na kudondokea kwenye kuni zilizokuwa karibu na nyumba yetu. Niliangalia upande mwingine wa nyumba yetu na kuona kijumba chetu cha bustani (greenhouse) kimeharibiwa kabisa. Paa lake la plastiki lilikuwa limeezuliwa kabisa. Nilichukua haraka simu yangu ili niangalie utabiri wa hali ya hewa, lakini mtandao ulikuwa umekatika.

“Mpenzi, tunaweza kuondoka?” Namsikia Natasha akiniuliza. “Ndiyo twenzetu,” niliitikia.

Tulimnyanyua Ethan aliyekuwa amelala kutoka kitandani, nikaweka kumpyuta mpakato yangu kwenye begi langu la mgongoni, kisha tukakimbilia kwenye gari na kuanza kuendesha tukihofia wakati wakati wo wote miti inayodondoka au inayopeperushwa ingeweza kutuzuia safari yetu. Tuliomba wakati tukitembea kwenye barabara iliyochafuka hadi kwenye nyumba ya wazazi wetu ambapo tulidhani pangekuwa salama zaidi kusubiria tufani iishe. Tayari kulikuwa na mti ulioanguka mbele yetu ambao tunashukuru tulifanikiwa kuukwepa.

Hadi sasa mvua ilikuwa bado inanyesha. Lakini licha ya mvua iliyokuwa inamiminika na upepo unaovuma tulifanikiwa kufika salama kwenye nyumba ya wazazi wetu. Jambo la ajabu ni kuwa. Hakuna yeyote kati yetu aliyetambua kuwa tufani ilikuwa inakuja. Mjomba wangu alikuwa kwenye trekta ikabidi aliache na kukimbilia ndani. Naye pia alikuwa na kijumba cha bustani ndani yake ambacho kiliezuliwa kama kile cha kwetu na kijumba kingine ambacho kilikuwa kimeharibiwa vibaya kiasi kilionekana kama tembo aliyechuchumaa. Dhoruba ilikuwa imetutandika bila kutarajia na bila kujiandaa.

Tunashukuru kwamba sote tupo salama na kila mmoja anaendelea vizuri. Lakini hata hivyo kimbunga kilitupiga bila kujiandaa. Ni sawa na vile ugonjwa huu wa COVID -19 ulivyoipiga dunia yetu bila kujiandaa. Hapa kuna jambo moja, tunatambua kuna vimbunga vinavyokuja kulingana na unabii wa Biblia. Swali ni je, “Tumejiandaaje kutuliza dhoruba hizo?” Ni kweli kuwa, kama mtunza bustani unatambua kuwa huwezi kutawala maumbile au asili. Upepo, mvua, jua, theluji – hayo yote huwezi kuyatawala. Unaweza kujipanga mapema na kujiandaa kwa ajili ya mambo hayo kama unao utabiri wa kuaminika wa hali ya hewa. Lakini nyakati fulani mambo ambayo hatukutarajia hutokea. Sasa hapo tunafanyeje?

Nitakueleza kile tunachofanya. Tunaomba. Tunatambua kwamba Mungu hutawala hata pale mambo yasiyotarajiwa yanapotokea. Hivyo tunanyanyuka na kusonga mbele. Wakati maisha yanapopukutika kutuzunguka pande zote, tunapaswa kunyanyuka na kuyajenga upya. Dhoruba za maisha zinaweza kutugonga hadi chini – lakini ni lazima tuinuke na kutafuta nguvu ya Mungu na kusonga mbele.

Kwetu sisi, kijumba cha bustani ilikuwa hasara ndogo. Ni kweli ilitugharimu fedha kidogo na muda wa kuitengeneza. Lakini ndani ya siku chache paa lilirudishwa mahali pake, na tunaamini wakati huu tumejiandaa vya kutosha, ikiwa hali ile itajitokeza tena.

Lakini vipi kuhusu dhoruba ya maisha? Vipi kuhusu dhoruba za kimwili, za kihisia, za kiroho, na za kiuchumi vilivyosababishwa na COVID-19? Unazijibuje changamoto hizo? Utafanyaje kujijenga upya? Unajifunza masomo gani yatakayokuandaa kwa ajili ya dhoruba zinazokuja? Wakati mambo yaliyo nje ya uwezo wako yanapotokea, unakimbilia wapi kupata nguvu na faraja?

Yesu ni nanga yetu na tumaini. Twaweza kumgeukia Yeye aliye Mfalme wa Amani atakayetuliza dhoruba kwa neno litokalo midomoni mwake. Twaweza kumgeukia ili atuvushe kwenye dhoruba ya maisha na hata katika nyakati za mwisho. Je, utamtegemea leo?

“Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini. Mtumainini Bwana siku zote Maana Bwana YEHOVA ni mwamba wa milele.” – Isaya 26:3-4

Siku ya 71, Ijumaa, Juni 05, 2020

MSWALI YA KUJIHOJI MOYONI: Umeupokeaje ugonjwa huu hatari ulioikumba dunia yote? Hali hii imeathirije au haijaathiri imani yako kwa Yesu? Je upo tayari kumtegemea Yeye kwa tufani zingine zisizotarajiwa zinazoweza kutokea maishani mwako? Unaamini kwamba Yesu aweza kuwa Mwamba wako wa kweli wa Milele?

CHANGAMOTO HALISI ZA MAISHA: Mwombe Mungu akuoneshe eneo lolote katika maisha yako ambalo huenda hujamkabidhi kikamilifu alishughulikie. Akuoneshe chochote ambacho hujisikii vizuri kumpatia akitawale. Mwombe akusamehe na akusaidie kumtumaini. Huenda ugonjwa huu hatari ulioikumba dunia yote umeibua mambo fulani maishani mwako ambayo ulionesha upungufu wa imani. Mwombe Yesu wetu mpendwa akusaidie kusalimisha yote kwake na ujifunze kumtumaini Yeye licha ya dhoruba za maisha.

TAARIFA ZA SIFA:

- **Alex G.,** anasema, "Mibaraka miwili mikubwa! Nimeanza masomo ya Biblia na tabibu kutoka mji wa kwetu. Na kwa sababu ya COVID-19 tutajifunza zaidi kuliko tulivyokuwa tunafanya huko nyuma. Amekubali kubatizwa hata kabla hajaja kanisani! Na mimi binafsi nimebarikiwa sana ingawaje imenipasa kusitisha safari zangu zote za mwaka kwa kuwa nitaweza kujipanga vizuri zaidi, nitaweza kuomba zaidi, kusoma Biblia zaidi, na kuandika zaidi na kufanya kazi kwa ufanisi. Katikati ya machungu mengi huja mibaraka mikubwa pia!"

- **Rebeca,** anasema, **"**Majuma mawili yaliyopita mume wangu na mimi tulikuwa katika mazingira magumu sana. Simu zetu hazikuwa zinapokea, na gari langu lilikuwa limekwama kwenye tope ambapo hapakuwa na njia yoyote ya kutoka. Tulimwomba Mungu awe rubani wetu. Nilipomaliza kuomba, nikajisikia kuimba wimbo. Mume wangu alisema nilipokuwa naimba alihisi kuna kitu fulani kilikuwa kinatusukuma kutoka pale tulipokwama. Nilitambua kuwa Mungu alikuwa anajibu maombi yetu. Ni Mungu wa kushangaza na ninapenda namna ambavyo daima anafanya kazi maishani mwetu!"

MAMBO YA KUOMBEA

- **Waombee** kaka na dada wanaopambana na hali ya kutoajiriwa katika kipindi hiki kutokana na gonjwa hili lililoikumba dunia yote.

- **Muombee** Magdalena na mumewe wanaoishi maeneo ya vijijini huko Kolombia wakijaribu kuwafikia watu ili wamjue Yesu. Wanahitaji jengo la kanisa mahali watakapokusanyika ili kuabudu.

- **Yaombee** makundi ya ulimwenguni kote, ambayo hayana mahali au jengo la kuabudia kutokana na mazingira mbalimbali.

- **Waombee** wamishionari wa kujitolea wa mwaka mmoja wanaowasaidia wahamiaji wa Kihaiti kule Chile wajifunze lugha ya Kihispania na wachukuliane na maisha na utamaduni wa Chile. Tafadhali muombe Mungu afanye kazi ndani ya wamishionari hawa wa kujitolea na kupitia kwao awasaidie kujenga urafiki na Imani.

Siku ya 72, Jumamosi, Juni 06, 2020

MSAIDIZI, WAKILI, MFARIJI

"Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu." – Yohana 16:7

"Roho Mtakatifu ilikuwa zawadi ya juu kuliko zote ambayo angeweza kuiomba kutoka kwa Baba yake kwa ajili ya kuwainua watu wake. Roho Mtakatifu alikuwa atolewe kama wakala wa kuumba upya, na bila [zawadi hii] kafara ya Kristo isingekuwa na faida . . . Dhambi ingeweza kuzuiwa na kuthibitiwa kupitia uwakala wenye nguvu wa nafsi ya tatu ya Uungu . . . Roho ndiye aletaye ufanisi juu ya kile kilichokamilishwa na Mkombozi wa Ulimwengu. Ni kupitia Roho ambapo moyo hufanywa safi. Kupitia Roho muumini huwa mshirika wa tabia ya Mungu. Kristo ametupatia Roho wake kama nguvu ya Uungu ya kushinda mazoea ya uovu tuliyoyarithi na yale tuliyojifunza na kutia muhuri kwenye kanisa tabia yake yeye mwenyewe. Kuhusiana na Roho Yesu anasema "Atanitukuza Mimi." – The Desire of Ages, p. 671

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:
Je, umewahi kuifurahia kikamilifu zawadi isiyoelezeka ya Roho Mtakatifu? Yeye ni sehemu ya wale watatu wa mbinguni. Alitumwa kwako kama zawadi kutoka kwa Yesu. Yeye huzungumza nawe, hukuongoza, hukushawishi, hukusaidia, hukufariji, hukubadilisha, na hukutia nguvu, kwenye safari yako ya mabadiliko ya kuwa kama Yesu alivyo.

Je, unajisikia vizuri kumwalika Roho Mtakatifu maishani mwako? Je, umeshamshuhudia "*akileta ufanisi juu ya kile kilichokamilishwa na Mkombozi wa Ukimwengu."?* Kwa nini usikubali zawadi ya Roho Mtakatifu kutoka kwa Yesu na kumwalika rohoni mwako, ukimpatia nafasi katika kila nyanja ya maisha yako?

SHUHUDA ZA SIFA

- **Nicole P.,** anasema, "Nimewaona watoto wangu wakikuza urafiki baina yao wenyewe kwa kadri wanavyo cheza na kufanya kazi pamoja bila kuwa na marafiki wengine. Tumekuwa na muda wa ziada wa maombi ya kifamilia ya asubuhi na jioni bila yeyote kukosekana eti kwa kuwa yupo kazini au shuleni. Tumefanikiwa kufanya kazi nyingi nyumbani kwetu tukiwa pamoja. Na tumekuwa na mazungumzo mengi ya maana ya kifamilia kuhusu matukio ya siku za mwisho."

- **Gabriel A.,** anasema, "Namshukuru Mungu kwa uponyaji maalum katika kipindi hiki cha siku 100 za maombi. Kiongozi wetu wa nyimbo wa Shule ya Sabato alitujulisha juu ya uponyaji wa ajabu wa mguu wake. Baada ya maombi Mungu akamponya na akaweza kuhudumu katika Sabato iliyofuatia ya Mei 23. Bwana Asifiwe!"

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** washiriki huko Nigeria walioathirika na mauaji na manyanyaso kutoka kwa majambazi mbalimbali na hata kutoka kwa maafisa wa eneo.

- **Ombea** mpango wa kujenga kituo kiitwacho Lifestyle Center kule huko Puncak, Magharibi ya Java. Muujiza wa fedha unahitajika!

- **Mwombee** Martina R. ambaye amekuwa akipambana na ugonjwa unaoshambulia kinga kwa miaka miwili. Ugonjwa wake umefanya iwe vigumu kwake kujikita zaidi kwenye kazi ya Mungu.

- **Ombea** kituo cha “Mianzo” kwenye visiwa vya Galapagos. Wanawafikia watalii kutoka kwenye majiji ya ulimwengu. Mianzo ndilo jumba la makumbusho la kwanza la kanisa la kwanza linalotumia teknolojia ya juu. Muombe Mungu aweke mkono wake juu yake, alete wageni, na kuwapatia wafanyakazi maneno anayotaka wawapatie wageni.

Siku ya 73, Jumapili, Juni 07, 2020

ROHO WA KWELI

"Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari." – John 16:13-14

"Kupitia Maandiko Roho Mtakatifu huongea na akili, na kuusadikisha ukweli moyoni. Hivyo huanika makosa, na kuyatupa nje ya moyo. Ni kwa msaada wa Roho wa Kweli, atendaye kazi kupitia Neno la Mungu, ambapo Kristo huwatiisha watu wake aliowachagua mwenyewe."– The Desire of Ages, p. 671

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Yesu ni Kweli. Yeye ndiye Kweli iliyofanyika mwanadamu. Kama muumbaji alitafsiri na kusimika uhalisia wote katika muafaka mkamilifu na tabia yake ya upendo usio na ubinafsi. Shetani aliingiza uongo na udanganyifu ulimwenguni, akijaribu kuusimamisha uhalisia mpya wa ubinafsi, ambao ni udanganyifu mwingine unaoongoza kwenye kifo. Ili kuepukana na udanganyifu wa shetani tumepewa Neno la Mungu. Roho Mtakatifu ndiye pekee awezaye kufungua macho yetu kwa ukweli wote wa Biblia kama ulivyo katika Kristo, aliye Kweli, Neno lililofanyika mwanadamu.

Je, utamruhusu Roho Mtakatifu amtukuze Yesu maishani mwako kwa kukuongoza kwenye Kweli yote? Je hutaishia katika kumruhusu tu kuufunua ukweli kwako bali pia utamruhusu aubadilishe moyo wako ili upatane na uhalisia na upendo usio na ubinafsi wa Mungu?

SHUHUDA ZA SIFA:

- **Vasantha P.:** anasema, "Kutokana na misukosuko hii ya COVID-19 nilipata muda zaidi wa kusoma Maandiko na kuandika niliyoyasoma, kusikiliza mahubiri, na kusikiliza nyimbo za kiroho. Hii imepelekea kuwa na muda nzuri ajabu ambao kamwe sijawahi kuwa nao!"

- **Carol D.:** anasema, "Ninamshukuru Mungu kwa huruma na wema wake. Nimekuwa Mwadventista Msabato kwa miaka 33, na ugonjwa huu ni mbaraka kwangu, kwa sababu sikuwa natambua umuhimu wa matengenezo ya afya. Mungu amekuwa akitenda kazi moyoni mwangu reform. Nimechagua kuwa mwanamatengenezo. Mungu atukuzwe!"

MAMBO YA KUOMBEA

- **Ombea** makanisa ambayo yanaendelea kupambana kubadilisha Huduma zao ziwe za kimtandao wanaokabiliana na uhaba wa vifaa vya kiufundi na changamoto za Huduma za kimtandao.

- **Ombea** Waumini wa Kiadventista wa Oman wanaohangaika kupata mahali pa kufanyia ibada baada ya ugonjwa huu wa Corona.

- **Ombea** familia zinazopambana na kukandamizwa na mapepo. Waombee wapate ushindi dhidi ya dhambi zinazoweza kuwa ndiyo mlango anaoutumia shetani kuwaingilia na kuwaharibu.

- **Ombea** mpango wa kupata nyumba ya Waadventista huko Leipzig, Ujerumani, itakayokuwa kituo cha kulelea wanawake wasio na makazi. Kwa zaidi ya miaka 25 huduma hii imewahudumia na kuwasaidia karibia wanawake 2,000. Tafadhali mwombe Mungu aendelee kusaidia Huduma hii, ikileta matumaini na uponyaji kwa wale wenye uhitaji zaidi.

Siku ya 74, Jumatatu, Juni 08, 2020

KUJISIKIA HATIA KUNAKOOKOA

"Akainama tena, akaandika kwa kidole chake katika nchi. Nao waliposikia, wakashitakiwa na dhamiri zao, wakatoka mmoja mmoja, wakianzia tangu wazee hata wa mwisho wao; akabaki Yesu peke yake, na yule mwanamke amesimama katikati. Yesu akajiinua asimwone mtu ila yule mwanamke, akamwambia, Mwanamke, wako wapi wale washitaki wako? Je! Hakuna aliyekuhukumu kuwa na hatia? Akamwambia, Hakuna, Bwana. Yesu akamwambia, Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena." – Yohana 16:8-11

"Ahadi ya Roho Mtakatifu haikomei kwa umri fulani au kwa utaifa fulani. Kristo alitangaza kuwa mvuto wa kiungu wa Roho wake ungekuwa na wafuasi wake hadi mwisho. Kuanzia siku ya Pentekoste hadi wakati huu, Mfariji ametumwa kwa wote waliojishusha kikamilifu kwa Bwana na kwa Huduma yake. Kwa wote waliompokea Kristo kama Mwokozi wao binafsi, Roho Mtakatifu huja kama mshauri, mtakasaji, mwongozi, na shahidi." – Acts of the Apostles, uk. 49

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Sehemu ya kazi ya Roho Mtakatifu ni kuthibitisha *dhambi, haki, na hukumu.* Mambo hayo matatu ya kuthibitisha yamewakilishwa katika hekalu na huduma zake. Pale ukumbini ni mahali ambapo kafara ya dhambi ilifanyika (ikielekeza kwa Yesu Msalabani); kwenye chumba cha Patakatifu mambo matatu yenye kutupa uzoefu wa *haki ya Kristo* tuipokeayo yalifunuliwa kupitia Meza ya Wonyesho (mafunzo ya Biblia), Madhabahu ya uvumba (Maombi), na Kinara cha taa (ushuhuda wenye kujazwa na Roho). Yote yakiwa kielelezo cha maisha ya Kristo yaliyo mfano wa maisha yetu leo; na katika Patakatifu pa Patakatifu tunakumbushwa umuhimu na uhalisia wa hukumu wakati Kuhani Mkuu atakapoingia mara moja tu Siku ya Upatanisho (Yesu akijikita katika hukumu ya upelelezi kwa niaba yako).

Kwa maneno mengine; kazi ya Roho Mtakatifu ni kukuongoza katika uzoefu wa wokovu kwa njia ya Imani katika kila jambo Yesu alilolifanya na analolifanya sasa kwa ajili yako. Je, unaweza kuona umuhimu na uzuri wa kazi ya Roho Mtakatifu? Je, kwa furaha waweza kuikumbatia kazi yake ya kukuthibitishia hali yako ya dhambi na kumruhusu siyo tu kukuongoza kwenda kwa Yesu, bali kukufanya ufanane naye katika tabia kama sehemu ya maandalizi ya hukumu?

SHUHUDA ZA SIFA:

- Makanisa mengi zaidi na zaidi yamefanikiwa kuinua kiwango chao cha mawasiliano ya kimtandao ili kuwafikia watu na kujiunga na jamii kupitia mitandao.

- **John K.:** anasema, "Inashangaza kwamba kupitia kipindi hiki cha taabu, washiriki wa kanisa katika eneo letu wamekuwa waaminifu zaidi katika kurudisha zaka na sadaka. Tulifikia kipimo chetu cha zaka tulichojiwekea cha mwezi Mei! Tunaomba asubuhi na jioni katika kipindi chote cha siku 100 za maombi. Hali hii siyo tu kwamba imepanda mazoea ya kuomba, bali pia imezidisha hayo mazoea nyumbani kwangu. Usiku wa jana

binti yangu mwenye umri wa miaka 2 aliniita akisema, “Baba, ni wakati wa kuomba!” Ninamtukuza Mungu na kutambua kwamba amepanda kile kilichokuwa kinakosekana kwenye familia yangu – mazoea ya kuomba.

MAMBO YA KUOMBEA

- **Omba** kwa ajili ya vijana na watu wazima wengi wanaopambana kujinasua na mazoea ya kuwa mitandaoni.
- **Ombea** washiriki wa Perth, huko Australia wanaofanya uinjilisti kwa njia ya barua za kwenye makasha (letterboxing) katika maeneo yao.
- **Mwombee** mtoto Tyson, wa huko New Zealand anayeishi kwa msaada wa mashine. Madakatari wanataka kuondoa mashine, lakini tunaamini Mungu anafanya kazi kwa kuwa ameanza kufungua macho, kutoa sauti na kusogeza miguu.
- **Ombea** kituo cha Adventist Life Hope kilichopo Nazareti. Kinatoa mafunzo ya Kiingereza, Kompyuta, na afya. Mwombe Mungu aibariki na kuikuza huduma hii, akiwakinga na kuwaongoza wafanyakazi ili waifikie mioyo.

Siku ya 75, Jumanne, Juni 09, 2020

KUAKISI TABIA YA YESU

"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria." – Wagalatia 5:22-23

"Wakati upokeapo Roho wa Kristo – Roho mwenye upendo usio na ubinafsi na atuhimizaye kufanya kazi kwa ajili ya wengine – utakua na kuzaa matunda. Neema za Roho zitaiva katika tabia yako. Imani yako itaongezeka, hali ya kujisikia mkosaji itazidi, na upendo wako utafanywa mkamilifu. Zaidi na zaidi utaakisi kufanana na Kristo katika yote yaliyo safi, yaliyo ya staha, yaliyo ya kupendeza . . . Tunda hili kamwe haliwezi kupotea, bali litazaa kwa aina zake mazao ya uzima wa milele." – Christ's Object Lessons, p. 67-68

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Roho hutuongoza kwa Yesu. Na kwa kadri tunavyodumu kuwa ndani ya Yesu kupitia muunganiko wa kila siku wa Roho Mtakatifu, atakuza ndani yetu tabia itakayoakisi kila siku tabia isiyo na ubinafsi, tabia ya kujikana nafsi, na tabia ya upendo wa Kristo. Ni mchakato wa mabadiliko ya maisha yote (ya kudumu). Kama ambavyo embe halitokei mara tu baada ya mbegu kupandwa lakini huchukua muda kukua hadi kuwa mti ambao hatimaye huzaa matunda, na ndivyo ilivyo pia kazi ya utakaso ni mchakato unaochukua muda. Lakini amini kwa hakika kuwa kwa njia ya kujisalimisha na kwa njia ya uaminifu kila nyanja ya tunda la Roho itakuwa wazi katika maisha yako!

Je, umemruhusu Roho Mtakatifu kukuza ndani yako tunda lake? Je, kuna Nyanja za tunda la Roho ambazo umekuwa ukimzuia asizifanyie kazi? Je, ni tamanio lako kuakisi Yesu zaidi na zaidi hadi pale watu watakachokiona kwako iwe ni tabia ya Yesu ya upendo iliyo ndani yako?

SHUHUDA ZA SIFA:

- **Jones S.:** anasema, "Namshukuru Mungu kwa ajili ya Siku 100 za Maombi. Zimeleta nuru maishani mwangu. Nimeanzisha kiwanda cha kuoka mikate cha Kiadventista katika kipindi hiki na ninasambaza Neno la Mungu kupitia uokaji wa mikate. Kupitia kazi ya Roho Mtakatifu mmoja ya watu waliopokea ujumbe ameamua kuwa Mwadventista Msabato. Namshukuru Mungu kwa kunionesha njia nyingi tunazoweza kusambaza Neno lake na kuharakisha kuja kwake!"

- **Brother P.:** anasema, "Kupitia nyakati za kufungiwa ndani, nilipitia hatua mbalimbali za kujihoji maswali kila juma, na Mungu akaniruhusu kupokea majibu kwa maswali yangu, kupitia jumbe mbalimbali na uzoefu wa waandishi wa Siku 100 za Maombi. Asante, Bwana, kwa upendo wako mkuu na kwa nyakati za kushiriki pamoja ulizoturuhusu kuwa nazo na ulimwengu nzima."

MAMBO YA KUOMBEA

- **Omba** kwa ajili ya wachungaji, wazee wa kanisa, na wainjilisti walei kote duniani waliojikita katika mahubiri ya aina mbalimbali mitandaoni.

- **Omba** kwa ajili ya makanisa ya Kiadventista ya huko Iceland. Kuna washiriki wachache na Iceland ni nchi ndogo sana. Ombea ubunifu wao wa uamsho na mavuno makubwa kwa ajili ya Yesu.

- **Omba** kwa ajili ya kituo cha Kiadventista cha kurekebisha waathirika wa madawa ya kulevya na ulevi katika jiji na makao makuu ya nchi ya Guatemala. Kando na kutafuta kufunguliwa kutoka mazoea ya madawa ya kulevya na ulevi, zaidi ya watu 1,500 wamebatizwa katika miaka 8 ya Huduma. Tafadhali muombe Mungu aendelee kubariki na kukipatia mahitaji kiyuo huku akibadilisha masha ya watu kwa umilele.

- **Omba** kwa ajili ya Mgahawa Mboga (Wasiotumia nyama) wa Waadventista huko Byron Bay, Australia. Upo katika nafasi ya 1 ya Migahawa inayopendwa na watalii huko Australia. Tafadhali omba ili kusudi Mungu abariki Huduma hii na kwamba kupitia Huduma hii aweze kuifikia mioyo yao.

Siku ya 76, Jumatano, Juni 10, 2020

ZAWADI BORA ZAIDI!

"Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" – Luka 11:13

"Bwana anaridhia zaidi kuwapa Roho Mtakatifu wale wanaomtumikia kuliko wazazi wanavyoridhia kuwapa zawadi nzuri watoto wao. Kila mtendakazi anapswa kupeleka ombi la kubatizwa kwa Roho Mtakatifu kila siku." – Acts of the Apostles, uk. 50

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Baba anaridhia zaidi sana kukupa wewe Roho Mtakatifu kama ukimuomba. Mungu huwa kamwe hatumii nguvu kuja kwako, ndiyo maana inakupasa kumuomba. Lugha ya asili katika Luka 11 huonesha kwamba uombaji huu ni wa kudumu, na ni shughuli ya maisha yote ya kutaka kuwa naye zaidi na zaidi, ukifunua moyo wako kwa Mungu kama maua yafungukapo kuelekea jua.

Daima na katika hali endelevu tunahitaji kuzamishwa na kujazwa na Uwepo wa Mungu kupitia Roho Mtakatifu. Kazi ya Mungu ya utakaso na maandalizi ya tabia kwa ajili ya umilele ni mchakato. Kila siku anatupatia udhihirisho mpya wa makosa yetu, changamoto zetu, na welekeo wetu, kupitia Neno lake, na tunahitaji kila siku kumwalika Roho wake mioyoni mwetu kwa ajili ya kupokea neema na uwezo wa kutii na kutenda mapenzi yake mema, na kuwapenda wengine yeye alivyotupenda.

Unaweza kuwa umewahi kuomba Roho Mtakatifu hapo nyuma, lakini kwa kuelewa kwamba unahitaji ubatizo wake wa kila siku, utaomba Uwepo wake zaidi maishani mwako? Je, utamwalika Roho Mtakatifu kila chumba cha moyo wako bila kuzuia chochote?

SHUHUDA ZA SIFA:

- **Luis U.:** anasema, "Mimi na mke wangu tumekuwa tukitumia Skype kujifunza Biblia na watu 6 katika kipindi hiki cha karantini. Niliwaalika watu wengi kutazama program maalum iliyokuwa inatangazwa na channel yetu ya Kiadventista nchini Brazil na watu wengi ambao hata siyo Wakristo sasa wanauelewa vizuri ujumbe wa Bwana wetu! Baadhi ya rafiki zangu ambao si Waadventista wameanza kuamini Kuja kwa Mara ya Pili kwa Kristo!"

- **Winfrida M.:** anasema, "Nataka kushiriki pamoja nawe neno la kutia moyo kwamba maombi yanafanya kazi! Sabato iliyopita watu watano walibatizwa huko Kinshasa kufuatia mpango wa Siku 100 za Maombi ambao ulisirikishwa redioni, kwenye WhatsApp na mitandao mingine ya kijamii!"

MAMBO YA KUOMBEA

- **Omba** kwa ajili ya washiriki waliorudi nyuma katika kipindi hiki cha Ugonjwa. Omba ili kusudi Roho Mtakatifu anene waziwazi mioyoni mwao. Omba kwa ajili ya wale watakaowatembelea wakajazwe ujasiri, hekima, na upendo wanapotafuta kuwasaidia kuurudia mwendo wa Imani pamoja na Yesu.

- **Omba** kwa ajili ya washiriki wa Konferensi ya West Zimbabwe wanaofanya matembezi ya kuwasaidia wahitaji, wanyonge, wazee, na walemavu katika jumuiya yao.

- **Omba** kwa ajili ya washiriki na/ washiriki wa zamani na vijana walionaswa kwenye mafundisho ya uwongo na yapotoshayo. Omba ili kusudi Mungu afungue macho yao na kanisa liwasaidie kuupata ukweli kama ulivyo kwa Kristo Yesu.

- **Ombea** ulinzi wa Mungu kwa wataalam wa afya wa CHI Memorial Hospital Chattanooga, na wa hospitali zingine kote ulimwenguni.

Siku ya 77, Alhamisi, Juni 11, 2020

KUWEZESHWA ILI KUHUDUMIA

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi." – Matendo 1:8

"Watumishi wa Mungu hawawi wote na vipawa vinavyofanana, lakini wote ni watendakazi wake. Kila mmoja anapaswa kujifunza kutoka kwa Mwalimu Mkuu, na kuwaambia wengine kile alichojifunza. Wote hawafanyi kazi moja, lakini chini ya mvuto utakasao wa Roho Mtakatifu, wote ni vitendea kazi vya Mungu. Mungu hutumia karama mbalimbali katika kazi yake ya kuongoa roho kutoka kwa jeshi la Shetani." – Ye Shall Receive Power, uk. 192

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Ni jambo la kusisimua kushiriki katika kazi ya Mungu ya kuwavuta watu kwa Yesu. Wewe ukiwa na talanta zako, uwezo wako, na mvuto wako unaweza kuwa wakala wa neema katika ulimwengu huu! Ni jambo la jabu kabisa! Wakati maisha yako yanaposalimishwa kwa Mungu, na umejazwa nan a Roho, atakuwezesha kufanya sehemu yako katika upendeleo wa kushangaza wa kuongoa roho! Atatakasa ustadi wako nan a kukupatia karama zake za kiroho ili kukamilisha kazi yoyote anayoiweka mbele yako.

Je utatoa muda wako kwa kazi ya kuongoa roho pamoja na Yesu? Je, unatumaini kuwa Roho Mtakatifu atakuwezesha kufanya hata yale yanayodhaniwa kuwa hayawezekani? Je, utamuomba Yesu akubatize kwa Roho kwa kadri unavyojihusisha kuufikia ulimwengu unaokuzunguka?

SHUHUDA ZA SIFA:

- **Mary F.:** anasema, "Kanisa letu limebarikiwa kwa kuunganishwa kwenye maombi katika Siku 100 za Maombi. Kanisa linahisi amani ya Mungu, na kanisa linaiona mikono yenye nguvu ya Mungu."

- **Ronald L.:** anasema, "Katika kipindi cha kufungiwa ndani kikundi kidogo ambacho kwa sehemu kubwa kilikuwa cha Waadventista waliorudi nyuma na wanaovutiwa na Waadventista walikuwa katika kujifunza Biblia kwa dhati. Kama mchungaji wao wa mtaa nilikutana na kikundi hicho kidogo, nikawaongoza katika huduma ya ibada ya uamsho. Mwishoni mwa mkutano tuliandaa Huduma ya kutawadhana miguu na Meza ya Bwana na kwa mshangao wetu jumla ya washiriki 52 walihudhuria katika Huduma ambayo, 60% ya wahudhuriaji walikuwa washiriki wa zamani na washiriki wapya waliompokea Yesu na waliofanya agano lao la dhati kupitia Huduma ya Meza ya Bwana. Ningependa kumtukuza Mungu kwa kuihusisha Papua New Guinea kwenye Siku 100 za Maombi siku ya 57. Mungu alijibu maombi yenu siku iliyofuatia ya tarehe

23 Mei kwa kuwaongoza kondoo wake waliopotea kurudi kwenye zizi lake. Mungu asifiwe!”

MAMBO YA KUOMBEWA

- **Omba** kwa ajili ya makanisa ya visiwa vya Caribbean ambako licha ya kuongoza katika kukabiliana na ugonjwa wa Corona, sasa hivi wanajiandaa kukabiliana na msimu wa kimbunga cha 2020.
- **Ombea** Huduma ya kanisa la Waadventista wa Sabato wa Ellicott City huko Marekani, wanaochangisha barakoa, glavu, na miwani kwa ajili ya wataalam wa afya.
- **Ombea** kanisa la Vijana la Setagaya ambalo linafanya kazi ya kujenga mahusiano na jumuiya inayowazunguka. Tafadhali waombee vijana na viongozi wao wanapotafuta mbinu ya kuokoa jiji lao.
- **Omba** kwa ajili ya kituo cha mvuto huko San Jose, Costa Rica, kinachotoa mafunzo ya muziki, mazoezi ya viungo, mashauri ya familia, madarasa ya Biblia na mengi mengineyo. Tafadhali mwombe Mungu abariki mpango huu wa ushuhudiaji na awalete watu wengi wanaopenda kumfahamu zaidi.